JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM

## SHAURI LA UKIUKAJI WA AGIZO LA SERIKALI KUHUSU KUTOSOMA HABARI ZA MAGAZETINI KWA UNDANI

## SHAURI NA. 05-2018/2019

## MAGIC FM RADIO

# UAMUZI

## UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA AGIZO LA SERIKALI LA KUTOSOMA HABARI ZA MAGAZETINI KWA UNDANI

### 1.0 Utangulizi

1.1 Kituo cha Utangazaji cha Magic FM Radio cha Dar es Salaam kinatuhumiwa kukiuka Agizo la Serikali lililotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe (MB), tarehe 03 Mei, 2017 kwa watangazaji wa vituo vya Redio na Televisheni kutosoma kwa undani maudhui yaliyomo katika magazeti badala yake wasome vichwa vya habari pekee. Kimsingi, agizo hilo la Serikali lililenga kulinda soko la biashara ya uchapishaji, usambazaji, na uuzaji wa magazeti nchini.

1.2 Aidha, tarehe 15 Juni, 2017, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) iliviandikia barua vituo vyote vya utangazaji (ikiwa ni pamoja na kituo cha Magic FM Radio) na kuvitaka kuacha mara moja kusoma kwa undani habari za magazetini na badala yake wasome tu vichwa vya habari kwa mujibu wa agizo hilo la serikali.

1.3 Kituo cha Magic FM Radio kinatuhumiwa kukiuka kwa makusudi agizo hilo la serikali kupitia kipindi chake cha "**Morning Magic**" kwenye kipengele cha "**Magazeti**" kilichorushwa mfululizo kuanzia tarehe 14 mpaka 17 Januari, 2019 kati ya saa 12.00 asubuhi na saa 04.00 asubuhi. Katika kipindi hicho, watangazaji wa kipindi walisoma kwa undani habari mbali mbali zilizoandikwa katika magazeti ya Uhuru, Mwananchi, Majira, Mtanzania, na Habari Leo kinyume na agizo lililotolewa na serikali.

1.4 Kitendo cha kusoma taarifa hizo za magazeti kwa undani ni kupuuza kwa makusudi agizo la serikali lililotolewa na Mheshimiwa Waziri tarehe 03 Mei, 2017

jijini Mwanza wakati wa kilele cha maadhimisho ya 26 ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari duniani.

1.5 Watangazaji wa kipindi cha Morning Magic walikiuka agizo hilo la Serikali kwa kusoma habari za magazetini kwa undani kama ifuatavyo:-

**Tarehe 14 Januari, 2019**

**Gazeti la Uhuru Uk.2:** *"Wazalilishaji watangaziwa kibano kikali; Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein ameiomba jamii kushirikiana na serikali katika mapambano dhidi ya vitendo vya uzalilishaji kwani vinadhalilisha jamii na vinafanywa kinyume na maadili.... Amesema vitendo vya uzalilishwaji wa wanawake na watoto bado vinaendelea kuripotiwa kila siku katika maeneo mbali mbali visiwani Zanzibar. Dkt. Shein aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Zanzibar katika sherehe za maadhimisho ya miaka 55 ya Mapinduzi zilizofanyika katika uwanja vya Gombani visiwani Pemba.Hii ni taarifa ambayo inapatikana katika ukurasa wa pili wa gazeti hili lakini pia"...*

*"Mamia wafurika kushuhudia uchomwaji wa sare za kijeshi; ni nguo 1947 zinazofanana na sare za kijeshi zimechomwa moto baada ya kubainika kuingizwa katika makambi ya wakimbizi mkoani Kigoma. Tukio hilo lilifanyika jana likishuhudiwa na mamia ya wakazi wa mji wa Kigoma, nguo hizo zilizoingizwa nchini kutoka nje kama mitumba zilikamatwa wakati wakimbizi wakigawiwa...Mkuu wa wilaya ya Kigoma Mjini Samson Hangaaliwaongoza viongozi wa vyombo vya ulinzi na usalama katika kazi ya uteketezaji wa nguo hizo ambazo zinafanana na zile zinazotumiwa na jeshi"*

*"Usiyoyajua kuhusu kondomu za kike hii hapa; ni pamoja na wataalamu kusisitiza umuhimu wa matumizi ya kondomu kama njia mojawapo ya kuepuka maambukizi ya ukimwi na magonjwa mengine. Baadhi ya wanawake hawapendi kutumia kondomu zao. Uchunguzi wa uhuru umegundua kwamba baadhi ya wanawake wameshindwa kujua namna zinavyotumika pamoja na kuwa na uelewa mdogo, pia baadhi ya wanawake wenye hali inayoridhisha kiuchumi wanatajwa kuwa ndio wenye uamuzi wa kutumia au kutotumia mipira hiyo ya kike wakiwa na wenza wao. Kuhusu wasio na kipato wanadaiwa kukosa uamuzi stahiki...Uhuru limezungumza na ofisa ustawi wa jamii wa hospitali ya taifa ya Muhimbili, Rose Mgene, ambaye alisema kondomu za kike huvaliwa kwa ndani elimu ambayo wanawake wachache wanayo ikilinganishwa na wengine wasiofahamu... Baadae wakati wa kupaka rangi taarifa hiyo maria ataipaka rangi ili aweze kutoa na elimu ya ziada Maria si unazijua vizuri Maria ... yes nazijua, uliwahi kuzitumia ... nazijua kwa sababu kazi yangu inanifanya nizijue. Swali ni kwamba uliwahi kuzitumia Maria?...sijawahi kuzitumia"*

*"Ashikiliwa na polisi akituhumiwa kumuuwa mwenzake; Jeshi la polisi mkoani Tanga linamshikilia mkazi wa Kibafuta huko kata ya Magokweni katika halmashauri ya jiji la Tanga aliyefahamika kwa jina moja la Mdoe akihusishwa na mauaji ya mwenzake...Kamanda wa polisi mkoa wa Tanga Edward Bukombe athibitisha kutokea kwa tukio hilo na aliwaambia waandishi wa habari kwamba ni kweli Jeshi la Polisi linamshikilia Mdoe akituhumiwa kumuua Juma Abeid."*

**Uk.3:** "*Dar, Pwani maji yapatikana kwa asilimia 95; ni Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka (DAWASA) imetangaza kumalizika kwa changamoto ya maji kwa asilimia 95 katika kipindi cha mwaka huu kwenye mikoa ya Dar es Salaam na Pwani Jumla ya sh. bilioni 115 zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya kumaliza tatizo hilo. Hili ni gazeti la Uhuru baada ya kuliangalia ukurasa wa kwanza mpaka wa nne naliweka pembeni.*"

**Gazeti la Majira**: "*Kanyasu atoa maelekezo kwa watumishi TAWA na TFS; ni Naibu waziri wa Maliasili na Utalii Costantine Kanyasu amewataka watumishi wanaopangiwa kufanya kazi katika mradi wa kufua umeme wa Mto Rufiji Stiegler's Gorge kufanya kazi kwa bidii na maarifa ya hali ya juu...Akizungumza katika pori la akiba la Selous katika kituo cha Mtambwe mkoani Morogoro baada ya kufanya ziara ya siku mbili katika eneo hilo kwa kutumia usafiri wa anga, barabara pamoja na majini Kanyasu alisema hatamvumilia mtumishi.*"...

"*Hospitali za rufaa kuimarishwa zaidi; Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na watoto Ummy Mwalimu amesema serikali imejikita kuhakikisha kila hospitali za rufaa zinakuwa na jengo maalum la kutoa huduma kwa ajili ya wagonjwa wa dharura.*"

"*Serikali yasisitiza umuhimu wa vituo vya mkono kwa mkono; Katibu Tawala mkoa wa Singida Dk Angelina Lutambi amewataka watendaji wa serikali mkoani Singida kuanzisha vituo vya mkono kwa mkono ili wahanga wa vitendo vya ukatili waweze kupata huduma kwa haraka tofauti na ilivyo sasa ambapo wanakumbana na mlolongo wa taratibu ambao unachangia kupotea kwa ushahidi.*"

**Uk.3:** "*Kunguni, Popo wa ajabu wawatibua wanafunzi huko Nkasi; Ni wadudu aina ya kunguni na popo wamevamia mabweni mawili ya wasichana katika shule ya Sekondari Kirando wilayani Nkasi Mkoa wa Rukwa na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wanafunzi hao...Akizungumza na majira Mwalimu Aloyce Nandi ambaye anafundisha masomo ya Kiswahili na uraia shuleni hapo alisema wadudu hao wasumbufu wamevamia mabweni ya wasichana wanaosoma kidato cha tano na sita shuleni hapo.*"

"*Uchumi wa Zanzibar waimarika, Rais Shein anena; Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohameid Shein amesema kutokana na juhudi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar za kuimarisha uchumi wake, ukusanyaji wa mapato umeimarika zaidi.*"

**Uk.4:** "*Serikali yapiga stop ubomoaji wa nyumba; Ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi amesema kuanzia sasa serikali ya awamu ya tano haitabomoa tena nyumba za wananchi walizozijenga maeneo ya makazi yasiyo rasmi na badala yake itarasimisha makazi holela...Waziri Lukuvi amesema Rais John Magufuli ametoa fursa kwa wananchi wote masikini waishio mijini waliojenga bila kufuata mipango miji na wasio na hati miliki za ardhi kufanyiwa urasimishaji wa makazi yao na wasibomolewe nyumba zao tena kwa kuwa hayakuwa makosa yao kujenga maeneo hayo.*"

"*Wabunge wa upinzani kutinga mahakamani sakata la CAG... ni wabunge watano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wametangaza kufungua kesi ya*

*kikatiba mahakama kuu ya Tanzania, masijala ya Dar es salaam kuitaka mahakama hiyo iwapatie tafsiri ya sheria juu ya mipaka ya kinga ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) pamoja na mamlaka ya Spika wa Bunge kuweza kumshtaki mwananchi bila kuathiri uhuru wa kutoa maoni kikatiba."*

**Gazeti la Habari Leo Uk.2:** *"Yajayo yanafurahisha ATCL... ni maboresho yanayofanywa na serikali katika shirika la ndege la ATCL yamezidi kuibua mipango mbali mbali ya shirika hilo yenye lengo la kuibua tija na kuongeza ufanisi ikiwa ni siku chache baada ya kuwasili kwa ndege ya sita aina ya Air bus. ...Ujio wa ndege hiyo unaifanya ATCL kuwa na ndege mbili za aina hiyo huku moja ikiitwa Ngorongoro na nyingine Dodoma."*

**Uk.3:** *"Mtanzania aibuka kidedea elimu ya juu; ni mwanafunzi Mtanzania Felister Rushubiza ameibuka kidedea baada ya kuongoza kitaifa matokeo ya elimu ya juu ya sekondari grade 12 ordinary level top ten yanayotolewa nchini humo...Felister (12) ni mtoto wa pili kati ya watoto wanne wa familia ya Joseph Rushubiza anayeishi nchini humo kwa takribani miaka 20."*

*"Lugola atumbua vigogo sita idara ya wakimbizi... ni waziri wa mambo ya ndani ya nchi Kangi Lugola amewasimamisha kazi viongozi sita wa idara ya huduma ya wakimbizi akiwemo mkurugenzi wa idara hiyo Haririson Mseke kwa madai ya uzembe uliosababisha ugawaji wa sare za kijeshi katika kambi za wakimbizi huko Kigoma."*

**Uk.4:** *"Maige kuwasilisha hoja bungeni Kiswahili kitumike kujifunzia... Mbunge wa Tabora Kaskazini Almas Maige anatarajia kuwasilisha hoja binafsi bungeni kuitaka serikali ibadili sera ya elimu na mafunzo kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu."*

*"Mufti ataka BAKWATA kubuni vyanzo vya mapato; Mufti wa Tanzania Abubakar Zuberi amewataka wajumbe wa halmashauri kuu ya Baraza la Waislamu (BAKWATA) kubuni vyanzo mbalimbali vya mapato ili kukuza uchumi wa taasisi hiyo ya dini nchini...Aliyasema hayo juzi wakati akifungua mkutano wa baraza hilo ulioanza juzi na kumalizika jijini Dar es Salaam na kusisitiza... "kwanza ikibidi hata wajumbe hao kutumia hata wataalamu waliobobea katika eneo hilo la kiuchumi ili kusaidia maeneo mbali mbali yaliyo chini ya BAKWATA."*

**Gazeti la Mwananchi Uk.2:** *"Wananchi waachana na nyama wakihofia ugonjwa wa kimeta; baada ya kubainika kuwa ugonjwa uliowakumba watu 81 na kati yao wanne kupoteza maisha ni kimeta, wakazi wa kijiji cha Nzoka wilayani Momba mkoani Songwe wamejawa na hofu ya kula nyama na kunywa maziwa na badala yake kutumia maharage na mboga mboga. Awali baada ya kuibuka, wakazi wa kijiji hicho walidhania kwamba ulileltwa na wachawi hivyo kuendelea kula nyama lakini baada ya majibu ya wataalamu kueleza ugonjwa huo unatokana na kula nyama yenye vimelea, jamii hiyo yote imeingiwa na hofu ya kula aina yoyote ya nyama."*

**Uk.3:** *"Lugola atoa agizo trafiki kupigana na dereva; wakati video inayoonyesha askari watatu wa kikosi cha usalama barabarani wakimshambulia dereva wa lori*

*ikizua gumzo mtandaoni jeshi la polisi mkoa wa Songwe limesema litatoa tamko la tukio hilo haraka iwezekanavyo. Katika video hiyo askari wanaonekana wakimshambulia dereva huyo kabla ya kundi la wananchi ambao walikuwa wakishangaa awali kuamua ugomvi huo. Alipoulizwa kuhusu tukio hilo Waziri wa Mambo ya Ndani Kangi Lugola alisema, "nimemtumia kipande hicho cha video Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani Fortunatus Muslim ili afuatilie kujua undani wake na taarifa itatolewa."*

*"Mama wa miaka 64 asimulia alivyopambana na mamba... Chibona Matoyo mwenye umri wa miaka 64 mkazi wa kijiji cha Kanyala wilayani Sengerema mkoani Mwanza amenusurika kifo baada ya kujeruhiwa na mamba wakati akioga katika Ziwa Victoria. Katika tukio hilo lililotokea Alhamisi iliyopita Chibona alivunjika mikono na kujeruhiwa paji la uso na sasa anapatiwa matibabu kwenye kituo cha afya cha Mwangwika wilayani Buchosa mkoani humo. Akizungumza na mwananchi jana mama huyo mwenye watoto watano na wajukuu tisa alisema wavuvi ndio waliookoa maisha yake baada ya kupiga kelele akiomba msaada."*

**Uk.4:** *"Lisu aanza ziara Ulaya atua Uingereza; Mbunge wa Singida Mashariki ChademaTundu Lissu ameanza ziara barani Ulaya na leo atakuwa London Uingereza ambako amesema ataeleza kwa kina kile alichoandika katika waraka alioutoa ...mwaka huu. Ziara ya Lissu inaanza baada ya Desemba 31 mwaka jana kuhitimisha safari ya matibabu aliyoianza Septemba7, 2017 baada ya kushambuliwa na watu wasiojulikana kwa zaidi ya risasi 30 mjini Dodoma muda mfupi baada ya kutoka kuhudhuria kikao cha mchana cha bunge."*

*"Sakata la CAG, Spika Ndugai lanukia Kortini.. ni wabunge watano wa upinzani wakiongozwa na Zito Kabwe wamepanga kufungua kesi Mahakama Kuu Kanda ya Dar es salaam kupata tafsiri ya kisheria kuhusu mipaka ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za serikali CAG na nafasi ya Spika wa Bunge kumshtaki mwananchi yeyote bila kuathiri uhuru wa kutoa maoni kikatiba. Zito ambaye pia ni Mbunge wa Kigoma Mjini ACT Wazalendo amewataja wabunge wengine kuwa ni Saed Kubenea(Ubungo), Athony Komu (Moshi vijijini) na Salome Makamba (Viti maalum) wote kutoka Chadema na Habibu Bombali Nchinga(CUF)."*

**Gazeti la Mtanzania:** *"Wadau wa muswada wa vyama vya siasa njooni... ofisi ya bunge mjini Dodoma imetangaza vikao vya kamati tatu za bunge kwa ajili ya kupokea na kusikiliza maoni ya wadau kuhusu miswada mitano ya sheria ukiwemo muswada wa marekebisho ya sheria ya vyama vya siasa ya 2018. Hata hivyo ofisi ya bunge imechukua hatua hiyo wakati vyama 10 vikiwa vimefungua kesi Mahakama Kuu kupinga muswada huo kupelekwa bungeni."*

**Uk.2:** *"Wanaharakati wakamatwa Loliondo; ni mtandao wa watetezi wa haki za binadamu wamelalamikia hatua ya jeshi la polisi mkoani Arusha kuendelea kuwashikilia Clinton Kairungi, Supuki Maoi katika eneo la Loliondo wilayani Ngorongoro. Kukamatwa kwa wanaharakati hao wa migogoro ya ardhi katika eneo la Loliondo hadi sasa bado hakujawekwa wazi. Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Onesmo Olengurumwa alisema hao ni watetezi wa haki za binadamu waliokamatwa Januari 7, mwaka huu kinyume cha sheria za nchi kwa kuwaweka rumande katika kituo cha polisi cha Loliondo hadi hivi sasa."*

*"Tafori, Sokoine kufanya utafiti wa miti; ni Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii Profesa Adolf Mkenda, ameagiza Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (Tafori) na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kufanya utafiti maeneo ilipoisha miti ipandwe mingine kwa ajili ya uvunaji wa haraka utakaoiingizia serikali kipato."*

*"Wananchi 700 wakosa huduma za maji Moshi... ni zaidi ya wananchi 700 wa taasisi ya elimu na afya katika vijiji vya Koresa na Uchira wilayani Moshi wamekosa huduma ya maji kwa zaidi ya wiki moja kutokana na kuibuka kwa mzozo kuhusu uhalali wa bodi mbili za maji...Wakizungumza na waandishi wa habari kijijini hapo walisema ni kwa zaidi ya wiki moja sasa hawana maji hali inayochangia wananchi kutembea umbali mrefu kutafuta maji."*

*"Dk Mwanjelwa ataka mafunzo bora kwa watumishi... Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Dkt. Mary Mwanjelwa amewataka watumishi wa chuo cha utumishi wa umma Tanzania kutoa mafunzo bora yenye kuzingatia weledi."*

*"Mbunge kuwasilisha maoni binafsi lugha ya kufundishia... Mbunge wa Tabora Kaskazini Almasi Maige amesema wakati umefika kwa watanzania kuanza kutumia Kiswahili kufundishia katika shule za sekondari na elimu ya juu kwa masomo yote. Amesema hatua hiyo itasaidia kuwawezesha vijana wengine kuelewa wanachofundishwa na kuwa na ufanisi katika utendaji kazi."*

*"Wananchi 650 wachunguzwa afya Pugu... wakazi 650 wa Pugu dampo wilaya ya Ilala jijini Dar es salaam wamefanyiwa uchunguzi bure wa afya wa magonjwa ya kisukari, shinikizo la damu, saratani ya matiti kwa wanawake, na macho kwa lengo la kutambua afya zao. Huduma hiyo imetolewa na taasisi ya Lions Club International katika zahanati ya Amanda Marga iliyopo eneo hilo."*

**Uk.4:** *"Zito, Kubenea kumnusuru CAG mahakamani... kiongozi wa chama cha ACT Wazalendo Zitto Kabwe na wabunge wengine wanne wanatarajia kufungua kesi ya katiba katika Mahakama Kuu ya Tanzania kumzuia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuitikia wito wa spika wa bunge. Hatua hiyo imekuja siku chache baada ya Zitto kuandika barua kwa Katibu Mkuu wa mabunge ya jumuiya ya madola CPA akimuomba kuingilia kati mgogoro unaoendelea baina ya Spika wa Bunge Job Ndugai na CAG Profesa Mussa Assad."*

**Tarehe 15 Januari ,2019**

**Gazeti la Majira:** *"Kesi ya muswada yatupiliwa mbali ni iliyofunguliwa na vyama 10 vya siasa vikiongozwa na zitto, mahakama kuu yakubaliana na hoja mbili kati ya 10 za serikali. Mahakama kuu ya Tanzania imetupilia mbali kesi ya kupinga muswada wa marekebisho ya sheria ya vyama vya siasa iliyofunguliwa na vyama 10 vya siasa nchini. Waombaji katika shauri hilo alikuwa ni kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, Kaimu Katibu mkuu bara wa chama cha wananchi (CUF) , Joram Bashange, na mkurugenzi wa habari, utetezi na mahusiano, CUF Salim Berman dhidi ya mwanasheria mkuu wa serikali."*

**Tarehe 16 Januari,2019**

**Gazeti la Habari Leo:** *"Benki M yamezwa na Azania ... Benki Kuu ya Tanzania BOT imehamisha mali na madeni ya Benki M kwenda Azania Bank Limited kutokana na kukabiliwa na upungufu mkubwa wa ukwasi hali inayosababisha Benki hiyo kushindwa kulipa madeni yake ikiwemo amana za wateja. Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es salaam jana, Naibu Gavana wa BOT Dr. Bernard Kibese amesema kuwa Benki M ilikuwa na madeni yanayofikia bilioni 618."*

*"JPM asitisha kuviondoa vijiji hifadhini... Rais John Magufuli ameagiza kusitisha mara moja hatua ya kuviondoa vijiji na vitongoji vinavyodaiwa kuwepo maeneo ya hifadhi ameagiza vijiji vyote 366 vilivyoainishwa kuwepo ndani ya maeneo ya hifadhi nchini visiondolewe katika maeneo hayo. Badala yake ametoa mwezi mmoja kwa viongozi wa wizara zote zinazohusika kubainisha maeneo ya vijiji hivyo na kuanzisha mchakato wa mabadiliko ya sheria ili yawasilishwe katika kikao kijacho cha bunge."*

**"***Bodi ya mikopo yakusanya shilingi milioni 94 kwa miezi sita... ni bodi ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu imevuka lengo la makusanyo kuanzia Julai hadi Desemba mwaka jana kwa kukusanya shilingi bilioni 94.01 huku lengo likiwa ni kukusanya bilioni 71.4 kwa kipindi hicho. Makusanyo hayo ni ongezeko la asilimia 8.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 85.88 zilizokusanywa kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2017 kwa lengo hilo la kukusanya bilioni 1.4."*

*"Magufuli ashinda tuzo ya viongozi katika siasa Afrika"... "Ni Rais John Magufuli ametangazwa kuwa mshindi wa tuzo za uongozi katika siasa iliyotolewa na jarida mashuhuli la African Leadership Magazine Tanzania kwa mwaka 2018. Jarida hilo la Uingereza limemtangaza Rais Magufuli kuwa mshindi wa tuzo hiyo kutokana na mafanikio ambayo Tanzania imepata chini ya uongozi wake. Na mchapishaji wa jarida hilo Dkt. Kenny Ngiami amebainisha kuwa Rais Magufuli amewapita asilimia 62.66 maraisi na viongozi wengine wa siasa hasa katika bara la Afrika walioingizwa kwenye shindano hilo."*

*"Kanisa kuwavalisha vitenge wasiovaa nguo za staha"* *Ni huko Mbeya waumini wa kanisa Katoliki parokia ya Ilomba jimbo kuu la Mbeya hawatoruhusiwa kuingia kanisani iwapo hawatatii agizo la kuvaa mavazi ya heshima yasiyodhalilisha utu wa mwanadamu."*

***"Katika ukurasa wa 4 wa gazeti hili****, Wananchi wafurahia mashamba ya Mohammed Enterprises kurejeshwa ni baada ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi juzi kutangaza kuyafutia hati ya umiliki wa mashamba sita yenye ukubwa wa ekari 1,2905.126 kati ya 12 ya mkonge yanayomilikiwa na kampuni ya Mohamed Enterprises Limited wilayani Korogwe Tanga. Baadhi ya wananchi wametoa ya moyoni kutoka na hatua hiyo."*

**Tarehe 17 Janauari ,2019**

**"Gazeti la Mtanzania... Katika ukurasa wa 2** *wa gazeti hili unakutana na taarifa kuhusiana na spika... tengua kauli yako ...ni kauli ya wapinzani..." "Kambi ya upinzani bungeni imemtaka spika wa bunge Job Ndugai kutengua uamuzi wake*

*wa kusimamisha vikao vya kamati za bunge ya hesabu za serikali PAC na kamati ya hesabu za serikali za mitaa LAC. Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana mwakilishi wa kambi ya upinzani John Mnyika alisema kauli aliyoitoa spika sio ya bunge bali ni yake binafsi. Haiwezekani mgogoro wa spika na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali CAG ukasimamisha mambo mengine ya bunge kuendelea kama kamati tunataka spika abadilishe uamuzi wake kwa kamati hizi mbili na awezeshe kamati hizo kukutana kabla ya tarehe 25 mwezi huu amesema Mnyika."*

*"JPM ateta na Dkt. Olesugun Obasanjo..., Rais Dkt John Magufuli amekuwa na mazungumzo na Rais Mstaafu wa Nigeria Dkt. Olesugun Obasanjo Ikulu DSM. Taarifa iliyotolewa na kurugenzi ya mawasiliano Ikulu kwa vyombo vya habari DSM jana ilisema baada ya mazungumzo hayo Dkt. Obasanjo alimpongeza Rais Dkt. Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya katika uongozi wake. Alisema moja ya kazi hizo ni kupambana na rushwa, kuimarisha utoaji wa elimu, kuimarisha miundombinu, kuongeza nishati ya umeme, kuboresha usafiri wa ardhini na angani na jinsi wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi wanavyopaswa kuelewa juhudi zinazofanyika."*

## 2.0 Wito wa kufika mbele ya Kamati ya Maudhui

Baada ya kuona ukiukwaji wa agizo hilo, tarehe 04 Aprili, 2019 Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa Magic FM Radio wito wa kufika mbele ya Kamati kutoa utetezi kwa nini wasichukuliwe hatua. Wito pia uliutaka uongozi huo ulete utetezi wa kimaandishi.

Tarehe 11 Aprili, 2019, saa 03:00 asubuhi, uongozi wa Kituo cha Magic FM Radio ulifika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao kwa nini kituo hicho kisichukuliwe hatua kutokana na tuhuma za kukiuka agizo la Serikali linalowataka watangazaji wa vituo vya Redio na Televisheni kutosoma kwa undani maudhui yaliyopo katika magazeti na badala yake wasome vichwa vya habari pekee. Katika kutoa utetezi wake, Magic FM Radio iliwakilishwa na Augustino Mganga, Meneja Ufundi, Fungo Emmanuel, Afisa Sheria, na Orest Kawau, Mtangazaji.

## 3.0 Kusikiliza Vipindi vya Morning Magic vya tarehe 14-17 Januari, 2019

Kamati ya Maudhui na Uongozi wa Magic FM Radio walisikiliza vipindi vya Morning Magic vya tarehe 14-17 Januari, 2019 vilivyorushwa na Magic FM Radio ili kujiridhisha iwapo kituo hicho kilikiuka agizo tajwa la Serikali au la.

## 4.0 Maelezo ya Utetezi ya Magic FM Radio

Uongozi wa Magic FM Radio uliwasilisha utetezi wao wa maandishi kwa Kamati. Katika utetezi wao huo, Magic FM Radio wamesema kuwa kwa sasa uongozi wa redio hiyo umebadilika na kwamba mmiliki mpya hana rekodi ya kupokea barua ya agizo la Waziri kutoka TCRA. Wameendelea kudai kuwa kosa wanalotuhumiwa nalo lilitendeka chini ya mmiliki wa zamani.

Magic FM Radio iliendelea kutoa maelezo ya utetezi wa mdomo kama ifuatavyo:-

4.1 **Fungo Emmanuel** ambaye ni Afisa Sheria wa kituo cha Magic FM Radio alianza kwa kukiri kuwa ni kweli vipindi vilivyosikilizwa na vinavyotuhumiwa kutumika kuvunja agizo la serikali ni vyao. Alieleza utetezi wao kama ulivyoandikwa kwa maandishi kuwa kwa sasa, Uongozi wa Magic FM Radio umebadilika kutoka mmiliki binafsi kwenda kwa Chama cha Mapinduzi (CCM) na kwamba uongozi mpya (CCM) hauna rekodi ya kupokea barua ya agizo la Serikali kutoka Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA). Aliendelea kueleza kuwa kosa wanalotuhumiwa nalo lilitendeka chini ya uongozi wa zamani na hivyo kama kutakuwa na adhabu basi mmiliki mpya atabebeshwa mzigo wa kosa lililotendeka chini ya mmiliki wa zamani.

4.2 **Orest Kawau** ambaye ni mtangazaji wa Magic FM Radio alianza kwa kusema kuwa wakati wa makabidhiano ya kituo, uongozi mpya haukukabidhiwa barua ya agizo la serikali kutoka TCRA na uongozi wa zamani. Hata hivyo, alieleza kuwa hata kama umiliki umebadilika, ni jukumu lao kuhakikisha kuwa maagizo ya serikali, sheria, kanuni, na taratibu za nchi zinazingatiwa ipasavyo.

4.3 **Augustino Mganga** ambaye ni Meneja Ufundi wa Magic FM Radio, alianza kwa kukiri kosa ambalo kituo chao kimelifanya hata kama uongozi umebadilika na hata kama hawana rekodi ya kupokea barua ya agizo la Serikali kutoka TCRA. Aliomba radhi kwa kosa lililofanyika na kuahidi kuwa halitojirudia tena na kwamba uongozi mpya utahakikisha kuwa Sheria, Kanuni, taratibu na maagizo ya Serikali yanafuatwa.

## 5.0 Majumuisho ya Utetezi

Katika kujumuisha utetezi wao, **Fungo Emmanuel** alisema kuwa anatambua kuwa tamko la Serikali ni halali na lazima lifuatwe. **Orest Kawau** alimalizia kwa kusema kuwa kabla ya kufika mbele ya Kamati wameshafanya jitihada zote za kuhakikisha kuwa wanazingatia agizo la Serikali katika vipindi .

## 6.0 Tathmini ya Kamati

6.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba kituo cha Magic FM Radio kupitia kipindi chake cha Morning Magic, kipengele cha Magazeti kimekiuka agizo la Serikali la kutosoma habari za magazetini kwa undani kwa makusudi na pia utetezi wake haukuwa wa msingi.

6.2 Kamati ya Maudhui imeona kuwa kubadilika kwa uongozi wa Magic FM Radio na kutokuwa na rekodi ya barua ya agizo la Mh. Waziri kama walivyodai sio utetezi wa msingi kwa sababu agizo hilo la Waziri lilitangazwa sana kwenye vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na Magic FM Radio yenyewe. Hata kama uongozi umebadilika, wafanyakazi wa Magic FM Radio ni walewale. Pia, **kutokujua** uwepo wa agizo la Serikali, Sheria na Kanuni sio utetezi wa msingi.

## 7.0 Ushauri wa Kamati kwa Magic FM Radio

Kutokana na udhaifu uliobainika Kamati inaushauri Uongozi wa Magic FM Radio kufanya mambo yafuatayo:

7.1 Kuimarisha na kuboresha usimamizi wa vipindi vyao.

7.2 Wafanye matayarisho ya kutosha ya vipindi vyao vya magazeti ili kuepusha makosa kama yaliyojitokeza.

7.3 Wawe mfano mzuri kwa redio nyingine katika kufuata Sheria, Kanuni, taratibu, na miongozo ya Serikali katika kazi zake kutokana na dhamana walionayo kwa sasa.

## 8.0 Uamuzi wa Kamati

Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa Magic FM Radio, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa kituo cha Magic FM Radio kupitia kipindi chake cha **Morning Magic** kimekiuka kwa makusudi agizo la Serikali la kutosoma habari za magazetini kwa undani kama ilivyoelezwa katika tathmini hapo juu.

Hivyo, Kamati ya Maudhui inaamua kukipa **Onyo Kali** kituo cha Magic FM Radio na kukiagiza kutorudia kosa kama hili.

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam siku hii ya tarehe **15** mwezi **Aprili**, mwaka **2019**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Bi Valerie Ndeneingo-Sia Msoka**

..................................................................

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Bwana Joseph Method Mapunda** ..........................................
2. **Bwana Abdul Ramadhani Ngarawa**..........................................
3. **Bwana Derek Kaitira Murusuri**..........................................
4. **Bwana Jacob Gregory Tesha**..........................................